# GAZETI RASMI LA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

**16 APRILI 2026**

***Hupigwa Chapa kwa Idhini ya Serikali na Imekubaliwa na Mkuu wa Posta kuwa ni Gazeti*** ***Hutolewa kila Ijumaa***

***Bei Tshs . 2000/=*** **CXXXV Nam. 7490**


**YALIYOMO** *Ukurasa*


Sheria ya Kutoza Kodi na Kubadilisha baadhi ya Kodi na Tozo na Kurekebisha baadhi ya Sheria zinazohusiana na Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato ya Umma na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.....683


## SEHEMU YA SHERIA

Sheria iliyotajwa hapo chini imetangazwa katika ***Gazeti Rasmi*** hili.

### Tangazo la Mswada

Nam: Mswada wa Sheria ya Kutoza Kodi na Kubadilisha baadhi ya Kodi na Tozo na Kurekebisha baadhi ya Sheria zinazohusiana na Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato ya Umma na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo

### TANGAZO

Mswada ufuatao utawasilishwa katika Mkutano wa Baraza la Wawakilishi utakaoanza tarehe 6 Mei, 2026 kwa kusomwa mara ya kwanza, pili na tatu na unachapishwa pamoja na Madhumuni na Sababu zake kwa ajili ya kutoa taarifa kwa wananchi.

ZANZIBAR (Ndugu Saleh Juma Mussa)

**16 Aprili, 2026** ***Kaimu Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi.***


**Matangazo yaliyohusu Waliofariki na Mali wa Watu waliofariki, kuvunja Mikataba ya ushirikiano, taarifa za Makampuni, Upotevu na marekebisho ya Nyaraka za Serikali na mengineyo ambayo ni muhimu kwa Umma lazima kuchapishwa katika Gazeti Rasmi. Nakala za Matangazo hayo zipelekwe kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar - Tanzania SLP 261 Maruhubi, Zanzibar. Nakala ziwasilishwe kabla ya Siku ya Alhanisi ya kila Wiki**

**MSWADA**

*wa*

**SHERIA YA KUTOZA KODI NA KUBADILISHA BAADHI YA KODI NA TOZO NA KUREKEBISHA BAADHI YA SHERIA ZINAZOHUSIANA NA UKUSANYAJI NA UDHIBITI WA MAPATO YA UMMA NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO**

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Fedha (Usimamizi wa Mapato ya Umma), 2026 na itaanza kutumika mara baada ya kutiwa saini na Rais.

Marekebisho ya sheria mbali mbali

**2.** Sheria zilizotajwa katika sehemu mbali mbali za Sheria hii zinarekebishwa kwa namna zinavyoelezwa katika sehemu husika.

## SEHEMU YA PILI
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA USIMAMIZI NA UTARATIBU WA KODI, NAM. 7 YA 2009

Kusomwa.

**3.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Usimamizi na Utaratibu wa Kodi, Nam. 7 ya 2009, ambayo katika sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 8.

**4.** Kifungu cha 8 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (2) kwa kufuta maneno "taarifa zinazohitajika kama zilivyotajwa katika kifungu cha 6" yaliyopo baina ya maneno "chini ya kifungu hiki" na "cha Sheria hii" na kuweka badala yake maneno "uthibitisho wa utambulisho".

Marekebisho ya kifungu cha 9.

**5.** Kifungu cha 9 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta kifungu kidogo cha (3) na kuweka badala yake kifungu kidogo kipya cha (3) kama ifuatavyo:

> "(3) Cheti cha usajili au nambari ya usajili wa kodi iliyotolewa chini ya Sheria hii itapaswa kuoneshwa muda wote pahali itakapoonekana ikiwa ni eneo halisi au la kidijitali katika eneo la biashara la mlipakodi."

Marekebisho ya kifungu cha 23.

**6.** Kifungu cha 23 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (7) kwa kuingiza maneno "isiyopungua Shilingi Laki Mbili na isiyozidi" kabla ya maneno "ya" na " milioni mbili".

Marekebisho ya kifungu cha 31.

**7.** Kifungu cha 31 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuongeza vifungu vidogo vipya vya (3) na (4) mara baada ya kifungu kidogo cha (2) kama ifuatavyo:

"(3) Mlipakodi anaweza, kwa maandishi, kuomba kwa Kamishna Mkuu kuongezewa muda wa kulipa kodi chini ya sheria yoyote ya kodi.

(4) Kamishna Mkuu anaweza, baada ya kupokea maombi na endapo ataridhika kuwa kuongeza muda ni muhimu kutokana na kutokuwepo kwa mlipakodi Zanzibar, maradhi au sababu nyengine za msingi, kuongeza tarehe ambayo kodi au sehemu ya kodi inapaswa kulipwa."

**8.** Kifungu cha 41 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (1) kwa kuongeza aya mpya ya (e) mara baada ya aya ya (d) kama ifuatavyo:

Marekebisho ya kifungu cha 41.

"(e) ambaye anafanya kazi kama muunganishaji ikijumuisha benki, kadi za malipo, watoa huduma za malipo ya kielektroniki na watoa huduma za malipo wengine waliothibitishwa kwa mlipakodi".

**9.**Kifungu cha 62A cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

Marekebisho ya kifungu cha 62A.

(a) kufuta neno "Kamishna" linalojitokeza katika kifungu kidogo cha (1) na kuweka badala yake maneno "mamlaka husika";

(b) kufuta kifungu kidogo cha (2); na

(c) kukipa upya nambari kifungu kidogo cha (3) kuwa kifungu kidogo cha (2).

## SEHEMU YA TATU
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA KODI YA ONGEZEKO LA THAMANI, NAM. 4 YA 1998

**10.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Nam. 4 ya 1998, ambayo katika sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Kusomwa.

**11.** Kifungu cha 16 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

Marekebisho ya kifungu cha 16.

(a) kuongeza kifungu kidogo kipya cha (4) mara baada ya kifungu kidogo cha (3) kama ifuatavyo:

"(4) Bila ya kujali sharti jengine lolote la Sheria hii, mlipakodi aliyesajiliwa na Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar anayetoa huduma za utalii au hoteli, hatakuwa na haki ya kupunguza kodi ya ununuzi inayotokana na upatikanaji au uingizaji wa huduma za ujenzi, vifaa vya ujenzi, ukarabati au uboreshaji wa bidhaa za mtaji, ikijumuisha jengo, vifaa vilivyofungwa, samani, vifaa au vyombo vya moto, endapo bidhaa hizo za mtaji zinatumika, au zinakusudiwa kutumika katika huduma za utalii zinazotozwa kodi."

(b) kuvipa upya nambari vifungu vidogo vilivyobaki ipasavyo.

**SEHEMU YA NNE**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA USHURU WA STEMPU, NAM. 7 YA 2017**

Kusomwa.

**12.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Ushuru wa Stempu, Nam. 7 ya 2017, ambayo katika sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 65.

**13.** Kifungu cha 65 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta maneno "tarehe 31 Disemba ya kila mwaka" yaliyopo mwisho wa kifungu kidogo cha (2) na kuweka badala yake maneno "baada ya miezi kumi na mbili kuanzia tarehe ya kutolewa".

Marekebisho ya kifungu cha 77.

**14.** Kifungu cha 77 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (3) kwa kufuta maneno "za usafiri wa kimataifa" yaliyopo mwisho wa aya ya (b).

**SEHEMU YA TANO**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA USHURU WA HOTELI, NAM. 1 YA 1995**

Kusomwa.

**15.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Ushuru wa Hoteli, Nam. 1 ya 1995, ambayo katika sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 3.

**16.** Kifungu cha 3 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kufuta kifungu kidogo cha (3); na

(b) kukipa upya nambari kifungu kidogo cha (4) kuwa kifungu kidogo cha (3).

**SEHEMU YA SITA**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA USHURU WA BIDHAA, NAM. 8 YA 2017**

Kusomwa.

**17.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Nam. 8 ya 2017, ambayo katika sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Kufuta na kuweka badala yake kifungu cha 18.

**18.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kufuta kifungu cha 18 na kuweka badala yake kifungu kipya cha 18 kama ifuatavyo:

"Msamaha kwa bidhaa zilizokamilishwa taratibu za forodha Tanzania Bara.

**18.**-(1) Bidhaa zilizoingizwa na kukamilishiwa taratibu za forodha Tanzania Bara hazitatozwa ushuru pale zitakapohamishiwa kwa matumizi ya Zanzibar endapo kiwango cha ushuru wa bidhaa kilichotumika wakati wa uingizaji Tanzania Bara ni sawa au kikubwa kama kiwango kinachotumika Zanzibar.

(2) Endapo ushuru wa bidhaa unaotumika Zanzibar ni mkubwa kuliko kiwango kilichotumika Tanzania Bara, tofauti ya ushuru wa bidhaa itachukuliwa kuwa haijalipwa na itakusanywa wakati wa kuhamishwa kwa bidhaa kuingia Zanzibar.”.

**SEHEMU YA SABA**
**SHERIA YA MAFUNZO YA AMALI,**
**NAM. 8 YA 2006**

**19.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Mafunzo ya Amali, Nam. 8 ya 2006, ambayo katika sehemu hii itajulikana kama “Sheria Mama”. Kusomwa.

**20.** Kifungu cha 27 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (3) kwa kufuta maneno “asilimia nne” na kuweka badala yake maneno “asilimia tatu”. Marekebisho ya kifungu cha 27.

**SEHEMU YA NANE**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA FEDHA (USIMAMIZI WA MAPATO YA UMMA), NAM. 9 YA 2015**

**21.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Fedha (Usimamizi wa Mapato ya Umma), Nam. 9 ya 2015, ambayo katika sehemu hii itajulikana kama “Sheria Mama”. Kusomwa.

**22.** Kifungu cha 20A cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (1) kwa kuongeza aya mpya ya (c) mara baada ya aya ya (b) kama ifuatavyo: Mareke-bisho ya kifungu cha 20A

“(c) usambazaji wa vifaa saidizi, vifaa tiba au vifaa vyenginevyo vilivyotengenezwa maalumu kwa matumizi ya watu wenye ulemavu.”

**SEHEMU YA TISA**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA UWEKEZAJI ZANZIBAR, NAM. 10 YA 2023**

**23.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Uwekezaji, Nam. 10 ya 2023, ambayo katika sehemu hii itajulikana kama “Sheria Mama”. Kusomwa.

**24.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 26A mara baada ya kifungu cha 26 kama ifuatavyo: Kuongeza kifungu kipya cha 26A.

“Matumizi mabaya ya msamaha wa kodi. **26A.**-(1) Mwekezaji ambaye amepewa msamaha wa kodi chini ya Sheria hii na akautumia vibaya msamaha, ametenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika:

(a) kulipa kodi ambayo ingeweza kulipwa iwapo msamaha usingetolewa; na
(b) kulipa adhabu ya asilimia hamsini ya kodi ambayo ingeweza kulipwa iwapo msamaha wa kodi usingetolewa.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, hakutakuwa na msamaha mwengine wa kodi utakaotolewa kwa mwekezaji huyo".

## SEHEMU YA KUMI
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA AJIRA, NAM. 11 YA 2005

Kusomwa.

**25.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Ajira, Nam. 11 ya 2005, ambayo katika sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 83.

**26.** Kifungu cha 83 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuongeza kifungu kidogo cha (5) mara baada ya kifungu kidogo cha (4) kama ifuatavyo:

"(5) Mwajiri atakayeshindwa kutoa nakala, marejesho na takwimu, ikiwa ni za vipindi au vyenginevyo za mikataba ya ajira, idadi ya wafanyakazi, viwango vya mishahara na masharti mengine yoyote ya utumishi yanayoathiri ajira hiyo, ametenda kosa na akitiwa hatiani atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Moja au kifungo kisichopungua miezi mitatu au adhabu zote mbili faini na kifungo".

## MADHUMUNI NA SABABU

Madhumuni ya Mswada huu ni kutoza na kurekebisha baadhi ya kodi na ushuru, na kufanya marekebisho ya sheria za fedha na kodi zinazohusiana na ukusanyaji na usimamizi wa mapato ya umma kwa ajili ya utekelezaji bora wa sheria hizo.

Kodi na ushuru zinazotozwa zinakusudiwa kukusanywa na mamlaka za kodi na kuwasilishwa katika Hazina ya Serikali kama mapato ya umma. Aidha, marekebisho ya sheria za kodi yanalenga kurahisisha taratibu za ukusanyaji wa kodi, kuzifanya sheria za kodi ziendane na hali halisi ya sasa, au kuongeza mapato ya Serikali bila ya kuathiri maslahi ya umma.

Mswada umegawanywa katika Sehemu Kumi:

***Sehemu ya Kwanza:*** ina masharti ya awali ambayo ni jina fupi na kuanza kutumika pamoja na marekebisho ya baadhi ya sheria.

***Sehemu ya Pili:*** inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi na Taratibu, Nam. 7 ya 2009 katika kifungu cha 8 (2), kifungu cha 23(7), kifungu cha 31, kifungu cha 41(1)(e), kifungu cha 62A pamoja na kufuta na kuandika upya kifungu cha 9(3).

***Sehemu ya Tatu:*** inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Nam. 4 ya 1998 katika kifungu cha 16 kwa kuongeza kifungu kidogo kipya cha (4).

***Sehemu ya Nne:*** inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa

Stempu, Nam. 8 ya 2017 katika kifungu cha 65 na kifungu cha 77.
***Sehemu ya Tano:*** inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Tozo ya Hoteli, Nam. 1 ya 1995 katika kifungu cha 3 kwa kufuta kifungu kidogo cha (3).

***Sehemu ya Sita:*** inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Nam. 8 ya 2017 katika kifungu cha 18.

***Sehemu ya Saba:*** inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Mafunzo ya Amali, Nam. 8 ya 2006 katika kifungu cha 27.

***Sehemu ya Nane:*** inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Fedha (Usimamizi wa Mapato ya Umma), Nam. 9 ya 2015 katika kifungu cha 20A.

***Sehemu ya Tisa:*** inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Uwekezaji Zanzibar, Nam. 10 ya 2023 kwa kuongeza kifungu kipya cha 26A.

***Sehemu ya Kumi***: inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Ajira, Nam. 11 ya 2005 katika kifungu cha 83.

ZANZIBAR (DKT. JUMA MALIK AKIL)
**16 APRILI, 2026** **WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO**
**ZANZIBAR**

LIMEPIGWA CHAPA NA WAKAL;A WA SERIKALI WA UCHAPAJI ZANZIBAR 2026